# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23.

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote**,** napenda kuchukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa Rehma, kwa kutujaalia afya njema na kuweza kukutana tena leo hii katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku kwa hali ya Amani na utulivu.

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa namna ya pekee, naomba nichukue nafasi hii kutoa pongezi maalum kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, kwa juhudi kubwa anazoendelea kuzichukua katika kuwaletea wananchi wa visiwa hivi maendeleo, katika mustakbali mzima wa kuijenga nchi na taifa kwa ujumla. Katika kipindi kifupi cha uongozi wake, Mheshimiwa Rais ameweza kufanya kazi nzuri ambayo kila mtu ni shahidi wa nafsi yake, na sisi kama Kamati tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya, nguvu, hekima na busara ili aweze kulitumikia Taifa la Zanzibar liweze kupiga hatua kubwa zaidi kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na pongezi hizo kwa Mheshimiwa Rais, pia tunampongeza Makamo wa Kwanza wa Raisi, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Raisi Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah, kwa juhudi zao kubwa katika kumshauri vyema Mheshimiwa Raisi katika harakati za kuieletea Zanzibar maendeleo pamoja na kujitoa kwao katika kuwahimiza wananchi kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Mheshimiwa Shamata Shaame Khamis pamoja na timu yake inayoongozwa na Katibu Mkuu, ndugu Seif Shaaban Mwinyi, Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Mheshimiwa Omar Said Shaaban, akisaidiwa na Katibu Mkuu wake Ndugu Ali Khamis Juma na Mheshimiwa Simai Mohamed Said, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale chini ya Katibu Mkuu wake ndugu Fatma Mabrouk Khamis. kwa kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu yao kwa maendeleo ya taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nichukuwe nafasi hii pia kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuipatia Kamati hii ushirikiano mkubwa ambao uliisaidia sana Kamati hii, katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Pamoja na shukurani hizo, Kamati pia inatoa shukurani kwa kupatiwa nafasi ya kueleza angalau kwa muhtasari, ripoti ya Kamati inayotokana na kazi zilizotekelezwa kwa takribani mwaka mzima.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 107(1) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2020 na majukumu yake yametajwa katika Jadweli la

Kwanza la Kanuni hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuyatekeleza majukumu haya, sina budi kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii kwa mashirikiano yao makubwa waliyoyaonesha katika kipindi chote cha Kamati, ambayo yamewezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi mkubwa.

Naomba niwatambuwe Wajumbe hao kama ifuatavyo:

1. Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi Mwenyekiti
2. Mheshimiwa Aza Januari Josseph Makamo Mwenyekiti
3. Mheshimiwa Mwanajuma Kassim Mjumbe
4. Mheshimiwa Nassor Salim Ali Mjumbe
5. Mheshimiwa Sada Ramadhan MwendwaMjumbe
6. Mheshimiwa Said Saleh Salim Mjumbe
7. Ndugu Mwaka Mwinyi Waziri Katibu
8. Ndugu Abubakar Mahmoud Idd Katibu

**Mjeshimiwa Spika,**

Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii inasimamia Wizara tatu, ambazo ni Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale. Kamati ilipata nafasi ya kufanya ziara kwa Unguja, Pemba na Dar es Salaam zikiwa na lengo la kufuatilia kwa kina utekelezaji wa Miradi na shughuli za Wizara hizo, ambazo hupangwa katika mfumo wa kibajeti wa Programu kama ifuatavyo:

## WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii katika kutekeleza majukumu yake ilifanya ukaguzi katika Programu Kuu za Wizara zifuatazo:

1. Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo;
2. Programu Kuu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu;
3. Programu Kuu ya Maendeleo ya Mifugo na
4. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

**Mheshimiwa Spika,**

Lengo kuu la programu hii ni kusimamia matumizi sahihi ya pembejeo na utoaji wa ushauri wa kitaalamu kwa wakulima, ikiwemo utoaji wa huduma za utibabu wa mimea, karantini na ukaguzi wa mazao. Aidha, programu ina jukumu la kusimamia na kuendeleza tafiti za kilimo na maliasili pamoja na upatikanaji wa huduma za Matrekta na Zana za Kilimo.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa programu hii, Kamati ilifanya ziara katika maeneo mbalimbali na kujionea hali halisi ya utekelezaji wa shughuli zinazoendelea katika maeneo hayo, ikiwa ni pamoja na Miradi ya Umwagiliaji maji kwa Unguja na Pemba, Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Chakula Dodeani kwa Pemba na Kizimbani kwa Unguja.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupata fedha za kugharamia ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji katika mabonde sita

kwa Unguja na Pemba. Lengo ni kuimarisha kilimo cha Umwagiliaji ili kujitosheleza kwa chakula.

**Mheshimiwa Spika,**

Hata hivyo, Kamati ilipofanya ziara katika mabonde ya Umwagiliaji, haikuridhika hata kidogo na utekelezaji wa baadhi ya miradi hiyo, hali iliyopelekea ufanisi mdogo kinyume na matarajio ya Serikali, ambapo fedha nyingi zimetumika na tija yake haijapatikana.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imeyabaini haya kwa mabonde ya zamani na yale ya sasa. Mifano mizuri ni kwa bonde la Umwagiliaji Chaani ambapo bonde limekamilika kwa asilimia mia moja lakini hadi leo bonde hili halijaanza kuwanufaisha wakulima kutokana na kukosekana kwa maji ya kumwagilia katika mashamba ya wakulima. Na kwa upande wa bonde la Umwagiliaji Machigini nalo halkadhalika, kwa mujibu wa maelezo yaliyopokelewa wakati Kamati ilipofanya ziara katika bonde hilo ni kwamba, bonde hili lilipitiwa na miradi tofauti ya maendeleo ikiwemo FAO, SMZ, TASAF na GSFP, miradi ambayo ilichangia kwa kiasi kikubwa katika upatikanaji wa fedha zilizosaidia katika ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji lakini hadi Kamati inafika katika maeneo hayo, imebaini kua tija ni ndogo kuliko matarajio ya wakulima.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, kuwa na usimamizi wa karibu sana wakati wa utekelezaji wa miradi kama hii ya maendeleo, hasa tukizingatia fedha nyingi za Serikali zimetumika. Aidha, Wizara ihakikishe kuwa, miradi inakuwa na viwango na ubora unaotakiwa, ili thamani halisi ya fedha iliyotumika katika miradi hii, iweze kuonekana na iweze kuwanufaisha wananchi kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na hali hii, Kamati pia ilibaini changamoto kubwa ya uharibifu wa Miundombinu ya Umwagiliaji, ambayo ujenzi wake uligharimu fedha nyingi. Wananchi wanaoishi karibu na mabonde hayo, huingiza Wanyama katika mashamba ya wakulima, jambo linalorudisha nyuma kasi ya maendeleo katika kilimo chao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kufuatia uharibifu huo wa Miundombinu ya Umwagiliaji katika mabonde hayo, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, kushirikiana na Kamati za ulinzi na usalama za Mikoa na Wilaya ambazo zitaweza kusaidia katika kuimarisha ulinzi katika mabonde yote. Aidha, jumuiya zilizopo katika mashamba hayo, ziandae kanuni ndogondogo zitakazotoa miongozo ya adhabu kwa wale wote watakaobainika kuingiza mifugo katika mashamba ya wakulima.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na umuhimu wa Miundombinu hii ya Umwagiliaji kwa wakulima katika mabonde yote yaliyopitiwa na Miradi hii, Kamati inaendelea kutoa ushauri wake kwa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, kushirikiana na Idara ya Kilimo kutoa elimu ya kutosha kwa jamii juu ya kuitunza, kuihifadhi na kuilinda miundombinu hiyo, Uwepo wa miundombinu hii ni hatua moja kubwa ya maendeleo katika sekta ya kilimo nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Mafanikio madogo yanayoendelea kupatikana kutokana na kilimo cha mpunga kwa njia ya Umwagiliaji ni changamoto nyengine iliyobainika wakati Kamati ilipokuwa katika ziara za kukagua kilimo hicho, hali inayochangiwa kwa kiasi kikubwa na uhaba wa upatikanaji wa pembejeo za

Kilimo kama vile mbolea. Wakulima huinunua mbolea hiyo kwa bei ya juu, kinyume na uwezo wao, matokeo yake ni kurudisha nyuma juhudi za wakulima hao katika kukiendeleza kilimo hicho.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mnasaba huu, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasli na Mifugo, kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa mbolea kwa njia ya ruzuku kutoka Wizara ya Kilimo ya Serikali ya Muungano wa Tanzania Bara, kwa lengo la kuwawezesha wakulima kutimiza ndoto zao katika kilimo hiki cha Umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na umuhimu wa kilimo cha mpunga nchini, Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara katika Mkoa wa Morogoro na kujionea hatua kubwa ya maendeleo katika kilimo hicho. Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mheshimiwa Fatma Mwasa pamoja na wasaidizi wake wote, akiwemo Afisa Tawala Mkoa, Mkurugenzi wa TARI pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mvumero. Miongozo sahihi inayoendelea kutolewa, imesaidia sana katika kuupeleka mbele Mkoa huu na kuwa kinara kwa uzalishaji wa mpunga kwa msimu wa 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, kuchota uzoefu, mbinu na maarifa ambayo wenzetu hawa wanayoyatumia katika kukiendeleza kilimo hiki, ili hatua kubwa ya maendeleo katika uzalishaji wa mpunga visiwani hapa

iweze kufikiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia ilipata nafasi ya kutembelea katika shamba la kilimo Tumbe na kujionea hali halisi ya uzalishaji katika shamba hilo, ambapo kwa msimu mzima wa kilimo, mavuno ya nazi katika shamba hilo hayaridhishi. Jumla ya nazi mia moja tu ndizo zinazovunwa kwa msimu mzima, hali iliyoitia wasiwasi mkubwa Kamati, hasa tukizingatia gharama kubwa zinazotumika katika kulihudumia shamba hilo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, kulikodisha shamba hili kwa watu binafsi waweze kuliendesha na kuepuka hasara inayoendelea kwa sasa.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii inasimamiwa na Idara ya Misitu ikiwa na jukumu la kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza rasilimali za misitu na wanyama pori pamoja na kusimamia uhifadhi wa misitu, mashamba ya Serikali, viumbe hai pamoja na mazingira yao, kusimamia mahitaji ya soko na matumizi endelevu ya rasilimali misitu.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa programu hii, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Misitu ya Mtambwe Kusini, Kaskazini pamoja na Msitu wa Masingini, ambapo Idara ya Misitu imeweza kuweka mahusiano mazuri kati ya wana vijiji vyote vinavyozunguka hifadhi za misitu hiyo. Idara ya Misitu kwa kushirikiana na Kamati za wana vijiji zinafanya juhudi kubwa ya kubuni vivutio vipya vya Utalii ndani ya misitu hii, ambavyo vitasaidia katika kuongeza mapato pamoja na idadi ya watalii wanaotembelea misitu hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika ziara yake hii, Kamati ilielezwa kwamba, Msitu wa Mtambwe Kusini na Kaskazini, Serikali ina lengo la kuipandisha hadhi Misitu hii kwa dhamira ile ile ya kuinusuru na uharibifu unaoendelea kufanyika siku hadi siku, ambapo mchakato wa upandishaji hadhi Misitu hii, ulianza mnamo mwaka 2020 kwa mashirikiano baina ya Idara ya Misitu na jamii ya Mtambwe Kusini na Kaskazini, ambazo ndio jamii zinazouzunguka Misitu hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Wakati hatua za kuipandisha hadhi Misitu hii zikiendelea, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Misitu Pemba, iendelee kuzishirikisha jamii zote zinazomiliki maeneo katika Misitu hii, ili kuepusha migogoro inayoweza kutokea hapo baadae, kati ya jamii hizo na Serikali.

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO**

**Mheshimiwa Spika,**

Lengo la programu hii ni kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake. Katika utekelezaji wake, programu imefanikiwa kuanzisha kituo cha kuhifadhia gesi ya upandishaji wa ng'ombe kwa sindano. Kituo hiki kwa kiasi kikubwa kimekua ni tegemeo kwa wafugaji katika shughuli zao.

**Mheshimiwa Spika,**

Changamoto kubwa katika utekelezaji wa programu hii ni uchakavu wa Mtambo wa kuzalishia gesi ya kupandishia ng'ombe kwa sindano, ambao ni wa muda mrefu sasa, hali inayopelekea kushuka kwa kiwango cha uzalishaji wa gesi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kupitia Idara ya Mifugo, kuharakisha mchakato wa manunuzi ya Mtambo huo, hasa tukizingatia kuwa bajeti yake tayari ipo.

## WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii katika kutekeleza majukumu yake kwa Wizara ya Biashara na Maedneleo ya Viwanda ilifanya ukaguzi katika Programu Kuu za Wizara zifuatazo:

i) Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda;

ii) Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali;

iii) Programu Kuu Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara;

iv) Programu Kuu ya Viwango na Tathmini na Ubora.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali utekelezaji wake unasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogovidogo, vidogo na vya kati (SMIDA), ikiwa na lengo la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda nchini, kuandaa na kusimamia utekelezaji wa programu na mikakati ya maendeleo ya viwanda na kufuatilia ukuaji wa sekta ya viwanda na utendaji wake, kwa kubaini vikwazo vinavyoikabili sekta hiyo na kuchukuwa hatua za kuziondoa.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa programu hii, mafanikio kadhaa yanaendelea kupatikana, ikiwa ni pamoja na ukuaji wa sekta ya viwanda na utendaji wake nchini. Kutokana na juhudi zinazochukuliwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda, kasi ya uwekezaji nchini imeongezeka, ambapo kwa sasa kisiwani Pemba viwanda kadhaa tayari vimeshajengwa na kuanza uzalishaji. Mfano Kiwanda cha Maji **AMOS INDUSTRIAL LTD** kilichopo katika Mji wa Viwanda Chamanangwe na Kiwanda cha Maji **WATER COM** kiliopo Kinyikani.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali kwa makusudi imetenga eneo maalum la uwekezaji katika eneo la Chamanangwe, ikilenga kutanua wigo katika sekta ya viwanda kisiwani Pemba. Kamati inaamini kuwa, uwepo wa viwanda vyote hivi, kutasaidia sana katika kupunguza makali ya ajira kwa vijana wengi nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Hata hivyo, Kiwanda cha Mwani kiliopo Chamanangwe kwa upande wake

nacho kipo katika hatua nzuri ya ujenzi wake, kukamilika kwake kutasaidia sana katika kuwakomboa wakulima wa mwani, ambao wengi wao ni wanawake wenye kipato cha chini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda pamoja na Kampuni ya Mwani kwa maamuzi yake ya kutoa vifaa vya kusaidia kilimo hiki kwa wakulima, jambo linalotoa hamasa na ari kubwa katika kukiendeleza kilimo hiki. Aidha, Kamati inaipongeza Kampuni ya Mwani kwa maamuzi yake ya kuanza kununua mwani aina ya Ulva ambayo kwa sasa unaonekana kuwa na matumizi makubwa duniani.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kupitia Kampuni hii ya Mwani, kutafuta soko la uhakika kwa aina hii mpya ya mwani, ili kuepusha mwani huu kujarundikana katika maghala.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali kupitia Wizara yake ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, haikuwa nyuma katika kuyatenga maeneo maalumu kwa ajili ya Maonesho ya Kibiashara nchini. Serikali imeamua kuyatenga Maeneo yanayotarajiwa kujengwa Viwanja vya Maonesho – Nyamanzi, yakilenga kuwakusanya wafanyabiashara wengi zaidi katika kuzitangaza biashara zao.

**Mheshimiwa Spika,**

Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda, kuongeza kasi katika kuhakikisha kwamba matengenezo ya viwanja hivyo yanakamilika kwa muda uliopangwa. Aidha, Idara ya Maendeleo ya Viwanda iendelee kutoa elimu zaidi kwa wafanyabiashara na wajasiriamali juu ya umuhimu wa kutafuta masoko na vifungashio katika kuzitangaza bidhaa zao ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Serikali na Wizara kwa ujumla, kwa hatua yake ya kuyafanya maonesho ya kibishara kuwa endelevu nchini. Maonesho haya ni muhimu sana katika kuzitangaza bidhaa ziliopo nchini ambapo inaendelea kutoa fursa kwa wajasiriamali wa ndani na nje ya nchi kuzitangaza bidhaa zao.

## PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara utekelezaji wake unasimamiwa na Programu ndogo tatu, programu ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji, Programu ndogo ya Uwezeshaji Biashara na Programu ndogo ya Utengamano wa Kibiashara, zikilenga kuweka mazingira bora ya biashara, kuongeza fursa za masoko pamoja na kurahisisha biashara nchini. Katika utekelezaji wa Programu hii, Kamati ilibaini changamoto kubwa ya mfumko wa bei kwa bidhaa muhimu nchini zikiwemo zile za mchele, unga wa ngano, sukari pamoja na mafuta ya kupikia.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kupitia taasisi yake ya Tume ya Ushindani Halali wa Kibiashara, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maghala na maduka kwa wafanyabiashara wote wakubwa na wadogo kwa lengo la kubaini changamoto ziliopo katika upandaji wa bei kiholela pamoja kuhakikisha kwamba wafanyabiashara hao wanafuata bei elekezi zilizowekwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya kipekee, Kamati inampongeza Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa maamuzi yake sahihi ya kukutana na wafanyabiashara nchini kwa lengo la kujadili suala zima la mfumko wa bei na upatikanaji wa bidhaa hizi visiwani hapa. Aidha, Mheshimiwa Rais kwa makusudi kabisa, aliamua kufanya ziara ya kushtukiza katika maduka mbalimbali kisiwani Pemba, kwa lengo la kubaini mwenendo mzima wa upatikanaji wa bidhaa hizi. Lengo ni kuirekebisha hali hii isiendelee kuwaathiri wananchi, ambao wengi wao ni wa vipato vya chini. ***Hivyo, Kamati yetu ya Kilimo, Biashara na Utalii inaendelea kumpongeza Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kujitoa kwake kwa maslahi ya Wananchi na Taifa kwa ujumla*****.**

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa muktadha huo, Kamati inaendelea kuwaasa wafanya biashara wote nchini kufuata sheria, taratibu na miongozo inayotolewa na Serikali. Kamati inayasema haya kutokana na ukweli kwamba, mfumko wa bei kwa bidhaa muhimu nchini unaonekana kuwa endelevu siku hadi siku, jambo linaloathiri maisha ya wananchi walio wengi. Wafanyabiashara wanatakiwa wajali zaidi maslahi ya wananchi waliowengi ambao ni wa kipato cha chini kuliko kujali kupata faida zaidi.

## SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC)

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilifanya ziara katika Shirika la Biashara la Taifa kwa Unguja na Pemba na kujionea maendeleo ya Shirika hilo pamoja na kukagua baadhi ya Miradi iliyo chini Shirika hilo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inalipongeza Shirika kwa hatua kubwa ya maendeleo katika kuliendeleza zao la karafuu nchini, kwa kuweka mazingira bora na rafiki katika vituo mbalimbali vya kuuzia na kununulia zao hili.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilifanya ziara katika kituo cha Wete na Mkoani Pemba na kujionea hali halisi ya mauzo kwa bidhaa hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu, ambapo Kamati ilijionea mazingira mazuri ya utoaji wa huduma hizo kwa wakulima wafikao vituoni humo.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na hali hiyo, wakulima walililalamikia Shirika juu ya upatikanaji wa daraja la kwanza kwa karafuu zao. Imekua sio kawaida kwa wakulima kupata daraja la kwanza kwa karafuu zao, maranyingi hupata daraja la pili na la tatu wakati wa mauzo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kupitia Shirika Lake la ZSTC, kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wakulima na jamii kwa ujumla, juu ya umuhimu wa kuzitunza karafuu kutoka hatua ya awali hadi hatua ya mauzo, lengo ni kufikia daraja iliyo bora zaidi wakati wa kuingia sokoni.

## WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Wizara ya Utalii na Mambo ta Kale, Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii katika kutekeleza majukumu yake, ilifanya ukaguzi katika Programu Kuu za Wizara hii kama hizi zifuatazo: -

1. Programu Kuu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe;
2. Programu Kuu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii;

3. Programu Kuu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii;
4. Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Kamisheni ya Utalii
5. Programu Kuu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Utalii.

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilipata nafasi ya kuyatembelea maeneo mengi ya kihistoria kwa Unguja na Pemba, na kubaini changamoto kubwa ya kukosekana kwa hati miliki kwa maeneo hayo pamoja na uvamizi mkubwa unaofanywa na baadhi ya wananchi kwa shughuli za kijamii ikiwa ni pamoja na kilimo na makaazi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na umuhimu wa hati miliki kwa maeneo haya ya kihistotia, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuharakisha upatikanaji wa hati miliki kwa maeneo yote ambayo hadi sasa bado mchakato wake haujakamilika. Kufanikiwa kwa suala hili kutaweza kuondosha kabisa migogoro pamoja na uvamizi kwa maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Wizara ya Utalii kupitia Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba, kwa juhudi zake inazoendelea kuzichukuwa katika kuibua vivutio zaidi vya Utalii kisiwani humo. Ongezeko la vivutio hivyo kutasaidia sana katika kuitimiza ndoto ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika kukitangaza kisiwa cha Pemba kuwa ni kisiwa cha Utalii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuendeleza mashirikiano yake na jamii yaliyosaidia kuvumbuliwa kwa vivutio hivi. Hata hivyo Wizara iendelee kutoa elimu ya kutosha kwa jamii juu ya umuhimu wa vivutio hivi nchini hasa tukizingatia kwamba, utalii kisiwani Pemba muamko wake unaendelea kuimarika.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kuendelea na kasi ya kuvivumbua, kuviendeleza na kuvitangaza vivutio vipya nchini kupitia vyombo mbalimbali vya habari kwa lengo la kutoa uwelewa kwa wageni wa ndani na nje ya nchi juu ya uwepo wake.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa napenda kukushukuru tena **Mheshimiwa Spika,** kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha muhtasari wa ripoti ya Kamati yangu kuhusiana na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale. Kamati imetoa ushauri na mapendekezo mbali mbali ambayo ni matumaini yetu kuwa yatafanyiwa kazi ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Niwashukuru pia wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati nikiuwasilisha muhtasari huu. Ripoti kamili ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii inapatikana katika vishkwambi vyenu Waheshimiwa wajumbe.

**Mheshimiwa Spika,**

Sasa niwaombe wajumbe wako waijadili kwa kina ripoti hii, kwa lengo la kuzisaidia Wizara zetu hizi ziweze kupiga hatua kubwa kimaendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Ahsante sana na naomba kutoa hoja.

**Ahsante,**

**Yussuf Hassan Iddi,**

**……………………………..**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii,**

**Baraza la Wawakilishi,**

**Zanzibar.**